

MAKTABA KUU-ZANZIBAR

KANUNI ZA KUJIUNGA NA UANACHAMA WA MAKTABA

- 1) Kila anaetaka kujiunga na uanachama wa maktaba atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo inapatikana katika dawati la mapokezi.
- 2) Fomu hiyo utatakiwa uirejeshe pamoja ikiwa na picha moja ya (passport size) itakayo tumika katika kutengenezea kitambulisho (IDENTITY CARD) ambacho utatakiwa kuwa nacho unapokuja kupata huduma za maktaba.
- 3) Fomu hiyo lazima iwe na muhuri halali wa skuli au muhuri wa sheha katika eneo unalotoka.
- 4) Utatakiwa kuandika namba yako au ya mdhamini wako ya simu ya halali kabisa, itakayotuwezesha kukupata pindi kukiwa na haja ya kufanya mawasiliano na wewe.

GHARAMA ZA UANACHAMA

- 5) Wanafunzi wa Vyuo TSH **5000/=**
- 6) Wanafunzi wa Secondary FIII-FVI **3000/=**
- 7) STDVII –FII TSH **2000/=**
- 8) STDI – STD VI TSH **1000/=**
- 9) WENGINEO TSH **5000/=**

KWA WAGENI

- 10) Wanafunzi wa Primary TSH **10,000/=**
- 11) Wanafunzi wa Secondary TSH **15,000/=**
- 12) WENGINEO TSH **20,000/=**
- 13) Uanachama utakaopewa utadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja tu ma utalazimika kuongeza muda wa uanachama uliopew kwa kulipia nusu gharama ulizolipa wakati wa kuomba uanachama.
- 14) Kila mwanachama atapatiwa kadi mbili (READERS TICKET) zitakazomuezesha kuazima vitabu viwili kwa wakati mmoja

KANUNI ZA UTUMIAJI WA MAKTABA

- 1) Hifadhi mikoba yako katika dawati la mapokezi, ni marufuku kabisa kuingia ndani ya maktaba na mikoba, mifuko au vifurushi.
- 2) Ni wanachama tu ndio watakoruhusiwa kuazima vitabu na idadi ya mwisho ya vitabu vya kuazima itakua ni viwili(2) kwa wakati mmoja.
- 3) Muda wa kuazima vitabu ni wiki mbili na baadhi ya vitabu ni wiki moja na lazima virudishwe si zaidi ya tarehe iliyoonyeshwa nyuma ya kitabu.
- 4) Iwapo mwanachama atahitaji kuongeza muda wa kukaa na kitabu/vitabu ni lazima avirejeshe maktaba kwa kuongeza muda.
- 5) Atakaecheleweshwa kurejesha kiitabu/vitabu atalazimika kulipa faini ya Tsh.200/= kwa siku kwa kila kitabu na hataruhusiwa kuchukua kitabu kingine akishindwa kulipa faini hiyo uanachama wake utasimamishwa hadi hapo atakapolipa faini hiyo.
- 6) Ikiwa mwanachama hatotumia uanachama wake kwa mwaka mzima, uanachama wake huo utakua umefutika.
- 7) Ni marufuku kuazima kitabu kwa kutumia kadi ya mtu mwingine.
- 8) Yeyote atakaebainika kuchukua kitabu kwa nia ya kuiba atachukuliwa hatua za kisheria.
- 9) Mwanachama atakaepoteza, atakaerudisha kitabu hali ya kuwa kimechanika au kupungua karatasi, atalazimika kukilipa kitabu hicho.
- 10) Sio ruhusa kuzungumza na simu unapokua Maktaba
- 11) Hairuhusiwi kula, kunywa, wala kuvuta sigara ndani ya Maktaba.
- 12) Ni marufuku kufanya majadiliano kwa sauti kubwa ndani ya Maktaba.

ZINGATIA :

- Unalazimika kufuata kanuni hizi wakati wote unapokua Maktaba
- Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakae vunja sharia hizi.

Tunaomba ushirikiano wako.

Kurejeshwa kwa fomu hii inathibitisha kuwa umezisoma ma kuzifahamu kanuni za utumiaji wa maktaba yetu na upo tayari kuzifuata